



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWA



Nambari ya Simu 023 2401045

Fax 023 2401046

Baruapepe. ded.kisarawe@pwani.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KDC/C.40/59/107

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Sanduku la Posta 28001,
28 Barabara ya Bomani,
61401 KISARAWA, KISARAWA
PWANI.

27 Machi 2024

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe amepokea kibali cha Ajira ya Mkataba chenye Kumb. Na. **FA.97/228/02"A"/131** cha tarehe 07 Februari, 2024 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hivyo anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wenye sifa na uwezo kujaza nafasi ya Afisa Usafirishaji Daraja la II

1.0. AFISA USAFIRISHAJI DARAJA LA II (NAFASI 1).

1.1. SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Shahada/Stashahada ya juu ya Usafirishaji kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

1.2. KAZI NA MAJUKUMU.

- i. Kutayarisha gharama za uendeshaji wa usafiri kwa ajili ya kusaidia kutoa maamuzi.
- ii. Kuhakikisha kuwa, takwimu na kumbukumbu zinazohusu vyombo vya usafiri pamoja na mitandao yake zinatunzwa vyema na kwa usahihi. Kuandaa takwimu zinazohusu mandeleo ya ukuaji wa Sekta ya usafirishaji, na kuwasilisha kwa watumiaji ndani na nje ya Nchi.
- iii. Kukusanya takwimu za usafirishaji Nchini.
- iv. Kukadiria na kushauri juu ya utendaji wa miradi mbalimbali ya sekta ya usafirishaji.
- v. Kutekeleza majukumu mengine yanayohusu sekta ya usafirishaji.

1.3. MSAHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali katika ngazi ya TGS D

2.0. MASHARTI YA JUMLA.

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na wasiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliojitosheleza Curriculum Vitae (CV) yenye anuani inayotumika, namba ya simu na anuani ya barua pepe (E.mail address) pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iii. Matokeo ya muda (Provisional/Testimonials/Statement of Result) havitakubaliwa.
- iv. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na mwanasheria/wakili.
- v. Waombaji waliostaafishwa katika utumishi wa umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na mwanasheria/wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne, kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na mamlaka husika (NACTE/TCU na NECTA).
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
- x. Waombaji wote waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) – Kwa ambao hawana vitambulisho, namba za NIDA ziandikwe kwenye maelezo binafsi (CV).
- xi. Mtumishi atakayeajiriwa atapewa mkataba wa mwaka mmoja (1). Anaweza kuongezewa mwaka mmoja (1) mwingine kutegemea na utendaji kazi wake (Renewable Once)**
- xii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa kutumia anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe,
S.L.P 28001,
KISARAWE.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 09 APRILI 2024 SAA 9:30 ALASIRI.

NB: Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ambayo ni www.kisarawedc.go.tz, mbao za matangazo Ofisi za Kata pamoja na tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz

Maombi ambayo yatawasilishwa kwa njia ya mkono hayatashughulikiwa.

Imetolewa na:

Beatrice R. Dominic
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE